

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

Simu: 028-2227148  
Nukushi: 028-2227140



Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P 20,  
**KARAGWE.**

Barua pepe: [ded@karagwedgec.go.tz](mailto:ded@karagwedgec.go.tz)  
Tovuti: [ded@karagwedgec.go.tz](mailto:ded@karagwedgec.go.tz)

***Unapojibu tafadhali taja:***

Kumb.Na.KGR/HWK/T.40/4/24

14/03/2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA UKUSANYAJI WA TAARIFA  
ZA ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI HALMASHAURI YA  
WILAYA YA KARAGWE**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe anapenda kuwatangazia wananchi wote kuwa kuna nafasi za ajira ya muda kwa ajili ya kukusanya taarifa za anwani za makazi katika vitongoji vyote vilivyoko katika Wilaya ya Karagwe. Kwa mantiki hiyo zingatia yafuatayo:-

**A. SIFA ZA MWOMBADI**

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 -35
- ii. Awe mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe
- iii. Awe na elimu ya kuanzia kidato cha nne na kuendelea
- iv. Awe anamiliki simu janja (smart phone) inayotumia Mfumo wa uendeshaji wa Android (Android OS) yenyewe uwezo wa kukaa na chaji siku nzima
- v. Awe na barua pepe (Email Address) na nywila (Password) inayofanya kazi
- vi. Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri ramani za kitongoji
- vii. Awe ni mkazi wa Kijiji/kitongoji husika
- viii. Awe tayari kufanya kazi katika kata yoyote ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe

## **B. KAZI NA MAJUKUU**

- i. Kujaza na kubandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- ii. Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- iii. Kukusanya taarifa za umiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia program tumizi ya Mfumo wa anwani za makazi
- iv. Kutumia data kwenye mfumo wa anwani za makazi
- v. Muda wa kazi utazingatia mkataba wa kazi

## **C. MAOMBI YAAMBATISHWE**

- i. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea
- ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- iii. Picha 2 za passport size
- iv. Barua ya maombi iliyopitishwa na Mtendaji wa Kijiji na Kata na wale walioko Mamlaka ya mji mdogo wa Kayanga barua zipitie kwa Mtendaji wa Kata

## **D. JINSI YA KUTUMA MAOMBI**

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu inayopatikana muda wote pamoja na barua pepe (E-mail) inayofanya kazi na kuwasilishwa ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Karagwe kwa anwani ifutayo

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P 20,  
**KARAGWE.**

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 18/03/2022 kabla au ifikapo saa 9:30  
Alasiri

Imetolewa na:-

  
Michael F. Nzyungu  
**MKURUGEZI MTENDAJI**  
**MKURUGEZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**KARAGWE**